

PASS TRUST



**PRIVATE AGRICULTURAL SECTOR SUPPORT TRUST
(ASASI YA KUSAIDIA SEKTA BINAFSI YA KILIMO)**

Mwongozo wa PASS



Taarifa kwa wateja na wadau wengine

Makao Makuu

Jengo la Patel, Ghorofa ya tatu, Mtaa wa Kisutu
S.L. P 9490, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110394, 2110395; Nukushi +255 22
2110392

Tawi la Morogoro (Ofisi ya Kanda ya Mashariki)

Jengo la National Audit, Ghorofa ya Pili
Mtaa wa Kitope, Karibu na Bwalo la JKT Umwema
S.L. P 146, Morogoro, Tanzania
Simu: +255 23 2613370/2613371/2613372; Nukushi
+255 23 2613373

Tawi la Mbeya (Ofisi ya Nyanda za Juu Kusini)

Jengo la NBC, Ghorofa ya kwanza
S.L. P 2921, Mbeya, Tanzania
Simu: + 255 25 250 0218; Nukushi: +255 25 250 0254

Tawi la Mwanza (Ofisi ya Kanda ya Ziwa)

Jengo la NSSF, Ghorofa ya Kwanza – Wing B,
Barabara ya Kenyatta
S.L. P 2098 Mwanza, Taanzania
Simu: +255 28-2505036; Nukushi: +255 28-2505036

Tawi la Moshi (Ofisi ya Kanda ya Kaskazini)


Lindi Lane, Jengo la Kibo Tower, Ghorafa ya pili,
Chumba na. 205, S.L.P 1987, Moshi, Tanzania
Simu : +255 27 2754760, Nukushi +255 27 2754760

Tawi la Mtwara (Ofisi ya Kanda ya Kusini)

Eneo la Shangani, Barabara ya TANU, Jengo la
Walimu, Ghorofa ya Kwanza
S.L.P 1395 Mtwara, Tanzania
Simu: +255 23 2334625; Nukushi +255 23 2334625

Barua pepe: pass@pass.ac.tz

Tovuti: www.pass.ac.tz





YALIYOMO

1. PASS TRUST ni nani?.....	3
2. Huduma zipi zitolewazo na PASS TRUST?	4
3. Nani anaweza kutumia huduma ya PASS?	5
4. Gharama.....	6
5. Jinsi ya kuomba na Wapi kwa kutuma maombi ya Huduma ya PASS?	7
6. Hatua zitakazofuatwa na Benki na PASS Trust kuhusu mikopo ambayo hairejeshwi kama ilivyopangwa.....	11



1. PASS TRUST ni nani?

PASS ni Asasi ya Kusaidia Sekta Binafsi ya Kilimo, PASS ni chombo kilichoanzishwa mwaka 2000 ili kuchochea uwekezaji na kukuza kilimo cha biashara na sekta zinazohusika. Ilisajiliwa mwaka 2007 kama Asasi isiyokuwa ya Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Ushirikishaji Wadhamini ya mwaka 2002.

DIRA


Kuwa asasi inayoongoza katika utoaji wa huduma za fedha na maendeleo ya biashara katika sekta ya kilimo.

DHAMIRA

PASS Trust/Asasi ya PASS inawajibika katika utoaji wa huduma za maendeleo ya kilimo cha biashara na fedha kwa wafanyabiashara wajasiriamali wadogo na wa kati kwa kuwaunganisha katika taasisi za fedha.

MALENGO YA PASS

Malengo ya PASS ni kuchochea uwekezaji na kuhimiza ukuaji wa kilimo cha biashara na biashara za kilimo nchini Tanzania.





2. HUDUMA ZIPI ZINAZOTOLEWA NA PASS?

Huduma zinazotolewa na PASS

- Huduma za maendeleo ya biashara
- Huduma za fedha



2.1 Huduma za Maendeleo ya Biashara za PASS

PASS inatoa huduma nyingi za maendeleo ya biashara kwa wateja kwa kuchangia gharama. Huduma hizo ni pamoja na:

- Upembuzi yakinifu.
- Kuandaa mipango ya biashara
- Kujenga uwezo; mfano katika maeneo maalumu ya kitaalamu.
- Kuwanganisha wakulima katika vikundi ambavyo vinaweza kutumika kama vikundi maalumu kwa ajili ya kilimo cha mkataba, kusambaza pembejeo kwa mkopo, kufanya mazungumzo ya bei na kutoa huduma ya ushauri.
- Utafutaji na uunganishaji wa masoko.



2.2 Huduma ya fedha

PASS itawasaidia watu na makampuni zinazostahili kupata mikopo kwa ajili ya uwekezaji wenye faida kupitia:

- Tathmini ya maandiko ya kuombea mikopo kulingana na masharti ya benki husika na kuunganishwa na benki hizo (Kwa sasa benki hizo ni: CRDB, NMB, EXIM, TIB, FBME, KCBL, BOA na ABC)
- Dhamana ya mkopo ambayo inatolewa kwa benki zenye mikataba ya kushirikiana na PASS Ili kujazia upungufu wa dhamana ya mteja




3. NANI ANAYEWEZA KUOMBA HUDUMA ZA PASS?

Mtu binafsi yeyote, Vikundi, chama au kampuni inaweza kutumia huduma za PASS, haswa:

- Wajasiriamali binafsi – ambao ni watu binafsi, vyama au kampuni zinazoshughulika na sekta ya kilimo
- Wajasiriamali binafsi – ambao wana dira na wanafanya biashara katika hali ya ufanisi na kibiashara.
- Wajasiriamali binafsi – watakaoshirikiana na PASS na benki washirika na kuwakilisha nyaraka zinazotakiwa na ambao wanaweza kufikia angalau vigezo vya msingi kwa ajili ya ukopaji

Kipaumbele kitatolewa kwa wateja wenye matokeo makubwa katika mwendelezo wa mnyororo wa thamani kwa bidhaa za kilimo hususani katika mazao ya chakula, biashara na mazao ya kusafirishwa nje ya nchi.




4. GHARAMA

Gharama za Huduma za Fedha na Maendeleo ya biashara za PASS zitachangiwa kati ya mwombaji na wadhamini wa PASS (PASS TRUST) kama ilivyoonyeshwa katika jedwali hapo chini:

GHARAMA ZA HUDUMA KUTOKA PASS

1. Kiasi Cha Mkopo Unaoombwa	Ada ya Maombi itakayolipwa
1.1 Mkopo chini ya Shilingi 100,000,000	50,000/=
1.2 Mkopo kati ya shilingi 100,000,000-500,000,000	0.05% ya Mkopo unaoombwa na kiwango cha ada cha Juu kitakuwa shilingi 250,000
1.3 Mkopo kati ya shilingi 500,000,000-1,000,000,000	0.05% ya Mkopo unaoombwa na kiwango cha ada cha Juu kitakuwa shilingi 500,000
1.4 Mkopo zaidi ya shilingi 1,000,000,000	0.5% ya kiasi cha dhamana inaoombwa na ada ya Juu itakuwa shilingi 5,000,000
2. Gharama ya Mchanganuo wa Biashara	2% ya Kiasi cha Mkopo unaoombwa

<p>3. Gharama ya Kukuunganisha na Benki</p>	<p>1% ya Kiasi cha dhamana inayotolewa na PASS nah ii ni kwa wateja wenye michanganuo yao ya Biashara inayokubalika na Benki. Ada hii inalipwa na mteja wakati ambao Benki imeshapitisha mkopo wake.</p> <p>Pia inalipwa na wateja ambao tayari wameshaanzisha na mahusiano na Benki husika lakini wanataka dhamana ya PASS ili Kupanua biashara na kupata Mkopo wanaohitaji.</p>
<p>4. Ada ya dhamana kwa wateja wakubwa</p>	<p>0.5% kwa kila robo ya mwaka(2% kwa mwaka) kwa kiasi cha dhamana itakayotolewa na PASS. Ada hii inalipwa PASS na mteja moja kwa moja.</p>



5. Jinsi ya Kuomba na Wapi kwa kutuma maombi ya Huduma za PASS?

Mwombaji atapaswa kujaza fomu inayotakiwa inayopatikana katika ofisi za PASS na benki washirika zilizopo karibu nawe na kuipeleka kwa benki yako yenye mkataba na PASS. Benki hiyo itapeleka ofisi za PASS Dar es Salaam/Mwanza/Mbeya/Morogoro/Mtwara/Moshi kwa ajili ya mchakato unaofuata. Mwombaji anaweza pia kupeleka nakala yake ya maombi moja kwa moja kati ya ofisi sita zilizotajwa hapo juu. Lakini PASS inasisitiza kwamba mwombaji awasilishe kwanza wazo lake la biashara katika tawi la benki lililopo karibu naye ili kutafiti kukubalika kwake.

Ni muhimu kwamba mteja / mwombaji kuwasilisha nyaraka zote muhimu kwa PASS/ mwakilishi wa benki washirika wakati wa maombi. Hii itaharakisha mchakato na kuzuia kupoteza muda kwa mteja.

Maombi yanapaswa kuwafikia PASS/benki washirika zinazohusika katika tawi lolote la benki washirika na kuomba fomu zinazohusika na taarifa nyingine na/au mwongozo muhimu wa kukamilisha hatua ya kwanza ya mchakato wa maombi.

Hatua ya awali: Mchakato wa maombi katika benki washirika:

- PASS / benki washirika zinazohusika zitapokea kutoka kwa mteja fomu ya maombi iliyojazwa, pamoja na nyaraka muhimu na uthibitisho wa malipo ya ada ambayo haitarudishwa.

- Uchunguzi wa awali wa uwekezaji utafanyika katika benki washirika
- Uwekezaji unaofaa utapitishwa katika ofisi mojawapo ya PASS kwa ajili ya hatua inayofuata.

Hatua ya kabla ya tathmini: Mchakato wa maombi katika PASS:

- Mteja atasajiliwa na PASS kwa kujaza fomu ya maombi ya PASS. Kuna aina mbili za fomu ya maombi: (1) Kwa ajili ya huduma za kifedha na (2) Kwa ajili ya huduma za maendeleo ya biashara. *Pamoja na fomu ya maombi, mteja anatarajiwa kulipa ada ya huduma anayohitaji.*
- Mteja atalipa ada ya PASS kupitia akaunti za benki zifuatazo;

Akaunti ya benki ya PASS Trust: CRDB PLC, Tawi la Morogoro

Namba ya akaunti: 01J1076972802

Jina la akaunti: Private Agricultural Sector Support Trust


Au

Akaunti ya benki ya PASS Trust: NMB, House branch

Namba ya akaunti: 22310001515

Jina la akaunti: Private Agricultural Sector Support Trust

- PASS na benki inayohusika kwa pamoja watamtembelea mteja kutathmini fursa ya biashara na dhamana ya mkopo. Katika hali maalumu ofisa





wa PASS atamtembelea mteja kabla ya benki inayohusika.

- Mteja atashauriwa kwenda katika benki kuomba kufanyiwa tathmini ya dhamana aliyopendekeza
- PASS na benki washirika watamjulisha mteja matokeo ya tathmini.
- Kama taarifa ya tathmini imekubalika, PASS wataingia katika mkataba rasmi na mteja ili kutoa huduma iliyoombwa. Katika hatua hii mteja anatarajiwa kulipa Ada yote ya mpango wa biashara kwa PASS. Baada ya malipo, PASS inaweza kuendelea na maandalizi ya mpango wa biashara. *Zingatia kwamba malipo ya ada hayamaanishi kwamba mkopo wa benki ni wa uhakika. Benki itakuwa mwamuzi wa mwisho wa kutoa au kukataa kutoa mkopo uliyoombwa*

Hatua ya Mpango wa Biashara: Maandalizi ya maombi yanayofanywa na PASS

- Mteja atalipa ada ya Mpango wa biashara (asilimia 2 ya mkopo ulioombwa) kwa PASS Katika namba ya akaunti ya CRDB au NMB kama zilivyotajwa hapo juu. PASS itaanda mpango wa biashara kwa kushirikiana na mteja. Kama mpango wa biashara utahakikisha kuwezekana kwa uwekezaji, PASS itamshauri mteja kuwasilisha katika Benki washirika kwa ajili ya kufikiriwa kupewa mkopo.

Hatua ya udhamini wa mkopo:

Baada ya benki kumkubali mteja pamoja na mpango wa biashara wa PASS, kutakuwa na mawasiliano zaidi kati ya

PASS na benki washirika kuhusu:


- Benki itafanya uamuzi kuhusiana na mkopo
- PASS na benki watakubaliana kuhusu kiasi cha udhamini wa mkopo
- PASS itatoa Hati ya Udhamini wa Mkopo katika Makao Makuu ya benki.

Hatua ya Utoaji wa Mkopo

- Benki itatoa mkopo na utaratibu wa urejeshaji- *pamoja na mapendekezo ya utaratibu wa kutoa mkopo kama ilivyo katika Mpango wa Biashara iliyoandaliwa na PASS.*

Hatua ya Baada ya Utoaji Mkopo

- Benki itafuatilia utaratibu wa marejesho na kutembelea mteja mara kwa mara na itakapowezekana watakuwa na mwakilishi wa PASS
- Benki itatoa taarifa kwa PASS kuhusu mabadiliko yoyote makubwa yanayoathiri urejeshaji wa mkopo wa mteja. Hili litahusisha mapendekezo ya utaratibu mpya wa urejeshaji mkopo na/au kupanga upya itakapolazimika



6. HATUA ZITAKAZOFUATWA NA BENKI NA PASS TRUST KUHUSU MIKOPO AMBAYO HAIREJESHWI KAMA ILIVYOPANGWA

Kama mteja ameshindwa kurejesha mkopo, benki watamtembelea mteja mara kadhaa kulazimisha urejeshaji wa mkopo. Hatua za ziada za kumrekebisha mteja zitatolewa kwa makubaliano kati ya PASS na benki inapobidi. Mwisho, kama jitihada zote zimeshindwa dhamana ya mkopo itauzwa kufuatana na makubaliano ya mkopo yaliyofanywa kati ya benki na PASS.



